



## **MADAI YA WANAMTANDAO WA KUPINGA MAPENDEKEZO YA MABADILIKO YA SHERIA YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA YA NGONO KIFUNGU CHA 10(b)**

Sisi Wanamtandao wa Kupinga Rushwa ya Ngono Tanzania na washiriki wote wanaopigania haki za binadamu na makundi ya pembezoni, kutoka takriban asasi 200 toka ngazi ya jamii hadi Taifa, tuliohusika na uchambuzi yakinifu wa mapendekezo ya awali ya marekebisho ya sheria hii na kutoa tamko letu kwa Tume ya Taifa ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Tunatambua sheria ya Kupambana na Kuzuia Rushwa ya Ngono, imetoa tafsri sahihi iliyotafautisha Rushwa ya Ngono na Rushwa nyingine. Kwamba Rushwa ya Ngono inahusisha **WENYE MAMLAKA KUTUMIA VIBAYA MAMLAKA YAO, KUDAI NGONO** kama sharti la kumpa mhanga haki na stahiki zake, au kumpendelea mhanga kwa kumwahidi kumtunuku vitu ambavyo hakustahili.

Rushwa ya Ngono ina athari nyingi kwa mhanga ikiwemo; kumpokonya na kudhalilisha utu wake, kumnyima fursa za kukuza vipaji vyake, kuendeleza kumfanya awe mtumwa wa ngono, kutoa nafasi za upendeleo kwa asie na sifa stahiki.

Rushwa ya Ngono huathiri kwa kiwango kikubwa uchumi wa taifa, pale ambapo inasababisha matumizi mabaya ya rasilimali watu, hivyo kudhoofisha jitihada za kupambana na umaskini, inahujumu utu wa taifa kwa kugeuza haki kuwa upendeleo kinyume na maadili ya utendaji kazi na kinyume na mikataba na makubaliano ya kimataifa na kikanda yanayokataza vitendo vya Rushwa ya Ngono.

Kwa kuzingatia matokeo ya tafiti zilizofanywa na TAKUKURU kwa kushirikiana na wanamtandao wanaopinga rushwa ya ngono, tunatambua ukubwa wa tatizo hili kwenye jamii yetu ikiwa ni pamoja na majumbani, (watumishi wa kazi za nyumbani wakiwa wahanga wakuu), mashulen, (wanafunzi na hasa wasichana wakiathirika zaidi), kwenye maeneo mengi ya utumishi wa umma na binafsi, maeneo ya biashara, kwenye hospitali zetu (hasa kwa wagonjwa wa kike), na hata kwenye taasisi za dini.

Tunatambua mwitikio wa elimu ya kuzuia na kupinga rushwa ya ngono umekuwa mkubwa kwa wazazi, watoto mashulen, vijana vyuoni, kwenye taasisi za kidini, waajiriwa majumbani na maofisini na katika tasnia ya Sanaa na utamaduni.

Hata hivyo, licha ya mafanikio haya, tumeshangazwa kwa kuendelea kupuuzwa kwa mapendekezo yetu, ya kufutwa kifungu cha nyongeza cha 25(b) Kilichompokanya mhanga haki, na badala yake kuongeza kifungu 10(b) kinachohalalisha kuendeleza matumizi mabaya ya mamlaka kwa njia ya kumhukumu mhanga wa rushwa ya ngono kama mbinu ya kuwanyamazisha na kuzima moto wa mapambano dhidi ya Rushwa ya Ngono.

Sisi wanamtandao tunaopinga rushwa ya ngono, tunatambua nyongeza ya kifungu cha 10(b) ni kinyume kabisa na sheria za Kimataifa, sheria za kuzuia Rushwa za SADC, Umoja wa Afrika na kanuni zote zinazoongoza Muungano wa Afrika Mashariki zinazokataza Rushwa ya Ngono.

**Hivyo basi,**

Sisi Wanamtandao unaopinga Rushwa ya Ngono, hatukubaliani kabisa na Marekebisho yaliyobainishwa kwenye kifungu cha 10(b) na tunapendekeza kifutwe kabisa kwani kinaenda kinyume kabisa na dhana nzima ya kifungu cha 25 cha sheria ya kuzuia na kupambana na rushwa. Na kinalenga kumlinda mhalifu badala ya kuwa msingi wa kuzuia uhalifu na kulinda haki.

Kwamba tunadai kifungu cha 25 kibaki kama kilivyo na kiendelee kutumika kwani kinajitosheleza bila kumbagua mhalifu awe wa kike au wa kiume.

**Kwa kauli moja, TUNADAI**

Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambalo linatuwakilisha sisi, lisipitishe haya mabadiliko, Kwani KAZI YA BUNGE NI KUTUNGA SHERIA ZA KULINDA HAKI NA SIO KUTUNGA SHERIA YA KUMLINDA MHALIFU. Na tunatoa wito kwa **WATANZANIA WOTE**, watetezi wa haki za binadamu, hususani za wanawake na watoto wa kike kupinga vikali kuingizwa kwa kifungu cha 10 (b) kwenye huu mswada.

Endapo Bunge litapuuza madai yetu, basi tunatoa wito kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dr. Samia Suluhu Hassan kukataa kuridhia haya mabadiliko yanayowasilishwa Bungeni kwa kuwa athari zake ni kubwa sana kwa Taifa letu.

**TUNALIKUMBUSHYA BUNGE: KURA ZETU NI TURUFU YA USHINDI WAO MWAKANI 2025.**

**TAMKO HILI LIMEANDALIWA NA MTANDAO WA KUPINGA RUSHWA YA NGONO TANZANIA.**